# Ee Mungu, unilinde

# Zaburi 15

siku ya Mungu ya 33 katika mwaka B

BYAMUNGU Michel




1. Bwana fungu la urisi wangu na la kiko**mbe** changu :
   ndiwe unayenilindia **ma**li yangu.
   Namweka Bwana daima mbele ya ma**cho** yangu;
   sitatikisika , kwa maana yupo kuume**ni** kwangu ;

2. Kwa hiyo moyo wangu waona furaha, nayo roho yangu yato**a** shangwe ,
   hata mwili wangu utapumzi**ka** salama.
   Kwani hutaiacha roho yangu ku**zi**muni ,
   wala hutamkubali mwamini wako aingie **shi**moni.

3. Ee Mungu , unilinde , kwa maana nakuki**mbi**lia.
   Utanionyesha njia **ya** Uzima,
   wingi wa furaha mbele ya u**so** wako ,
   anasa za milele kuume**ni** kwako.

*Kigali , le 9 novembre 2024*